

**BENKI KUU YA TANZANIA**  
16 Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Simu: +255 22 223 3167  
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



**BANK OF TANZANIA**  
16 Jakaya Kikwete Road  
P.O. Box 2303  
40184 DODOMA  
**TANZANIA**

Phone: +255 22 223 3167  
Email: botcommunications@bot.go.tz

**22 Oktoba 2023**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **MFUMO WA KIELETRONIKI WA USAJILI NA USIMAMIZI WA VIKUNDI VYA KIJAMII VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA NA WAHAMASISHAJI WA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kufahamisha Umma kwamba kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imefanya maboresho kwenye mfumo wa mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya halmashauri (TPLMIS) kwa kuongeza moduli za usajili na usimamizi wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha (Community Microfinance Groups) na Wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha (Microfinance Business Promoters). Mfumo huu ulioboreshwu wa kielektroniki unalenga kuwezesha vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha kuwasilisha maombi ya usajili na taarifa za uendeshaji kwa njia ya kielektroniki kuitia tovuti <https://www.mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz>.

Mwongozo wa kuwasilisha maombi ya usajili na taarifa za uendeshaji wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha kuitia mfumo wa kielektroniki pamoja na fomu zinazohusu maombi ya usajili vimewekwa kwenye tovuti ya mfumo huu kwa ajili ya rejea kwa watumiaji. Hivyo, vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha wanashauriwa kuendelea kuwasilisha maombi ya usajili na taarifa za uendeshaji katika halmashauri husika kuitia mfumo huu mpya ili yaweze kufanyiwa kazi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia tarehe 23 Oktoba 2023.

Benki Kuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wizara ya Fedha inapenda kuwakumbusha vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha na wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha ambao hawajasajiliwa kuhakikisha kuwa wanasajiliwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, kikundi chochote au mhamasishaji kuendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha bila kusajiliwa ni kinyume na matakwa ya sheria, hivyo hatua stahiki zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

Aidha, ikiwa watumiaji wa mfumo watapata changamoto wanashauriwa kuwasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii, Mratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha au Afisa TEHAMA aliyepo katika Ofisi ya Kata au Halmashauri iliyo karibu kwa ajili ya msaada zaidi. Vilevile, wanaweza kuwasiliana na kituo cha huduma kwa mteja katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa namba zifuatazo (**Nambari za Simu: +255262 160 210 na +255735 160 210 au Tuma ujumbe kwa whatsapp namba: +255735 160 210**).

**GAVANA  
BENKI KUU YA TANZANIA**